


# Kusafisha Kijito

Imechochewa na Kisa Halisi Cha Maisha


Mawandishi: Olivia Wood
Tafsiri: Mourice Wabwire
Mchoraji: Francine Tuczynski

ASHOKA
Worldreader

*“Kusafisha Kijito”*, ni hadithi ambayo imechochewa na kisa halisi cha maisha ya mvulana mdogo kutoka taifa la Brazili aliyeshangazwa na wingi wa taka ndani na kando kando pa mto uliopo karibu na kwao. Akidhamiria kuchukua hatua, aliwahimiza wanajamii kushirikiana katika kusafisha mto na kurejesha urembo wake wa asili.

Kitabu hiki cha picha cha watoto ni tukio la ushirikiano baina ya Ashoka na shirika la Worldreader. Kinalenga kuwahamasisha watoto kila mahali kuwa wanamageuzi na kuwahimiza watu wazima kuwaunga mkono katika safari hiyo.

Mto Araguaia ni moja ya baadhi ya mito mikubwa nchini Brazili. Ni maakazi ya maelufu ya wanyama, kwa mfano Kasuku wa samawati na manjano. Pomboo wa mto huogelea na kucheza kwenye maji, na pia kuna samaki wengi wa rangi.




Katika mji mmoja, mvulana wa miaka kumi na mitatu ajulikanaye kama Rhenan anatembea kando ya mto. Lakini kwa kutazama mto huo inampa hofu kwa sababu ya takataka zilizotapakaa kote. Anaona chupa za plastiki, nguo mzee na masalio ya karatasi za kuhifadhi vyakula. Maji yanaonekana kuwa machafu sana.



Shuleni, Rhenan anauliza kuhusu mto uliochafuka. “Haungependa kuwe na taka nyumbani kwako,” alisema mwalimu wake. “Hebu tafakari kuwahusu masikini wanyama wanaoshi hapo!”

Kwa siku kadhaa, Rhenan hakusita kufikiria kuhusu ule mto. Haikuonekana vyema kuwa mto huu mkubwa na wenye umaarufu umejazwa na taka. “Inawadhuru wanyama walioko karibu hapa,” anafikiria. “Pia inazidhuru familia zinazoishi hapa.”


Basi Rhenan lilimjia wazo.



Asubuhi iliyojiri, Rhenan alizungumza na mamake juu ya mpango wake kuhusu mto. Anataka kuzunguka mji anakoishi na kuwaomba wote msaada. Labda, iwapo wote wangeweza kushirikiana wanaweza kuusafisha mto!

.

Mamake Rhenan analipenda wazo hilo, “Ninaamini kitu cha maana kwako wewe Rhenan, ni kujifunza jinsi ya kuleta mabadiliko kwa vitu ambavyo unavyovijali. Hilo utakuwa nalo milele.” Anamhakikishia kuwa atamsaidia hadi mwisho.



Siku iliyofuata, Rhenan anaenda katika kituo cha polisi. Kisha anaenda kwa afisi ya mkuu wa jimbo. Anazuru shule nyingine nyingi, afisi na biashara kadhaa.

Punde anapata kikundi kikubwa sana cha watu wanaoungama na wazo hilo! Wote wanakubaliana kukutana mtoni wiki ijayo.

Siku ya kusafisha mto, Rhenan licha ya kuchnagamaka tu bali pia alikuwa na wasiwasi sana. Je, itakuwaje iwapo watu hawatajitokeza?

wakati yeye na mamake wanawasili pale mtoni, tayari kulikuwa na watu takribani mia wakiwemo rafiki za Rhenan.



Kwa siku nzima, wote wanafanya kazi kwa pamoja kuokota takataka. Wanokota kando kando pa mto na kuvuta zingine kutoka majini.

Wanapomaliza, walikuwa wameokota takribani tani moja ya takataka- huo ni uzito sawa na gari dogo!


Wanapofanya kazi Rhenan anagundua jinsi kila mmoja anacheka na kutabasamu. “Ni vyema kusaidia jamii yetu,” alifikiri.



Wanapomaliza kusafisha, wanapiga gumzo katika kundi moja kubwa. “Tunataka kukomesha jambo hili kutendeka tena,” alisema mwanamke.


Wanajamii wanaamua kuanza na elimu. Wanataka kuelimisha kila mmoja kuhusu hatari za kutupa uchafu katika mto.

Pia wanapanga kuusaidia mto kwa kupanda miti mingi kando kando iwe mkaazi ya ndenge na wadudu.



Mwisho wa siku, kila mtu alitoa shukrani. Wanajivunia mageuzi ambayo wameleta, nao mto wenye maji masafi ukitiririka kando yao.

“Hatungefanikisha shughuli hii pasipo nyinyi,” walimwambia Rhenan. “Asante sana kwa kutuhimiza kuleta mageuzi! Tufanye nini kingine tena kwa pamoja?”



# MATUKIO

ASHOKA | Worldreader

**Tukio 1: Matembezi ya kusikiliza**
**Kundi-umri: umri wote**
Ujuzi: Huruma, Kusikiliza kwa makini
Nyenzo: Hakuna

**Mbona?**

Katika historia ya wanadamu, mtu hutarajia kuishi pahala pamoja na kufanya kazi moja, huku akijumuika kimsingi na watu wenye dini na tamaduni moja. Dunia ya sasa inatulazimu sote tuwe na huruma: Sio uwezo tu wa kuhisi hisia za mwenzako bali kuzielewa pia. Hicho sicho kitu cha aidha kuwa nacho au kutokuwa nacho, pia si kitu ambacho mtu anaweza kujifunza kwa muda wa lisaa limoja na kuhifadhiwa katika kumbukumbu. Badala yake, kukuza huruma ni baadhi ya mazoezi ya kila siku. Mazoezi yanaweza kufanyika mahali popote, kwa kuwasikiliza wenzako na kutazama watu na vitu vilivyokuzingira.

Vipi?

Nenda kwa matembezi ya kukisikiliza na familia yako. Mhimize kila mmoja kusikiliza na kutazama vitu vilivyoko kando yake. Shindeni mkisimama simama. Safarini, ulizaneni maswali kwa ukaribu bila ya kumhukumu mwenzako. Badilisha nafasi kwa yule anayeongoza kikundi ili kila mmoja apate nafasi ya kuongoza matembezi.

Baadhi ya maswali ambayo ungeyauliza ni:

1. Je unasikia nini?
2. Je, ukidhani wadudu ama ndege wanafanya nini unachosikia?
3. Je, ni sauti zipi unazozisikia kutoka kwa wanyama?
4. Je, ni sauti zipii unazozisikia kutoka kwa binadamu?
5. Je, mwili wako unahisi vipi sasa hivi?
6. Je, kelele hizi zinakufanya ufikirie nini?

**Tukio 2: Matembezi ya Mageuzi**
**Kundi-umri: Umri wote**
Ujuzi: Huruma, Heshima
Nyenzo: mfuko wa takataka, glavu

**Mbona?**
Huwezi kujifunza kuwa mtu mwenye huruma ukiwa umejitenga; ni sharti iundwe na wazazi,wakufunzi, ndugu na rafiki. Uandazili wa modeli ya wanamageuzi pamoja na watoto huwezesha watu wazima kuwa mfano mwema huku wakidhibitisha katika hali halisi ya maisha jinsi tukio moja ndogo huleta mabadiliko makubwa. Kufanya mazoezi kwa pamoja kama familia ama darasa huimarisha misuli ya kuleta mageuzi kwetu sote.

**Vipi?**
**Baada ya matembezi ya kusikiliza, tafakari kuhusu mazingira yako kwa mfano, nyumba, mtaa na majirani. Ni mtaa upi, ua gani au mto upi unaoweza kusafisha kwa muda mfupi kila siku? Fikiria, je Rhenan angefanya nini? Nenda kwa matembezi mengine na familia yako ama rafiki zako. Okota na utupe takataka ili ung'arishe kijiji chako.**

Maswali ya kujadiliana:
- Je ulihisi vipi ukitupa takataka ulizoziokota?
- Je, mbona ni muhimu kuokota taka?
- Rhenan aliwakaribisha marafiki na majirani kumsaidia kusafisha mto uliopo karibu na nyumbani kwao. Tunawezaje kuwahimiza wengine kuokota taka ili kurembesha mazingira?

Tukio 3: Kitabu changu cha Hadithi ya Mageuzi
Kundi-umri: 3-8
Ujuzi: Ubunifu, Mageuzi
Nyenzo: Karatasi, Kalamu, Kalamu ya alama, vifaa vingine vya sanaa

Mbona?

Hadithi huipa changamoto dhana zetu za awali, kutuwezesha kuwa katika hali sawa na wale ambao wana changamoto tofauti na zetu. Ni kupitia hadithi ndiposa watoto hupata fursa ya kuwa katika ulimwengu dhahania, na kukumbana na wahusika, mazingira na matukio ambao hawatawahi kuyapitia. Pindi tu wanapozaliwa, watoto huanza kujiona kama wahusika wakuu wa hadithi zao, na kuanza safari na tabia za wahusika ambazo wanazisoma.

Vipi?

Mtu yeyote wa umri wowote, anawezaleta mabadiliko chanya. Tazama picha za hadithi za awali. Jichukulie kuwa mwanageuzi kama Rhenan. Rhenan anajali sana mito; je, wee unajali zaidi nini? Je, kitabu chako cha hadithi kingefanana vipi? Hebu toa mchoro wa jalada la kitabu chako cha hadithi, huku ukionyesha lile wazo la kufanya shule ama jamii bora. Ipe hadithi mada. Jadili mchoro wako na watu watatu tofauti unaowajali kwa mfano ndugu, babu au nyanya ama mwalimu. Pia jadili nao hadithi ya Rhenan ili wasome na kujifunza kutoka kwake.

Baadhi ya maswali ya kutafakari:

1. Ni changamoto ipi yenye wewe ama mpendwa wako ameipitia iliyokuumiza ama iliyokupa huzuni?
2. Ni nini baadhi ya sababu za kutokea kwa changamoto hizo?
3. Ni mambo yapi umeyasikia ama kuyasoma kuhusu ambayo ungependa kujifunza zaidi kuhusu?

## Mfahamu Rhenan:



Safari ya Rhenan ya mageuzi ilianza na usafishaji wa mto Brejinho,mkondo mdogo unaojiunga na mto Araguaia karibu na mji wake wa nyumbani Brazili. Mto huu unalinda na kutoa mahitaji ya kimsingi kwa maelfu ya wanajamii, usambazaji wa maji kwa mashamba, miji na mfumo wa ikolojia. Kama kijana, Rhenan alitambua utegemeano wa watu na dunia, na kutunza vyote vinahitaji kila mmoja kuchukua hatua. Sasa hivi, anawashawishi vijana wenzake kutia fora katika kuyatunza mazingira na kulinda ikolojia katika taifa zima la Brazili.

## Kuhusu Ashoka

Ashoka anaamini kuwa uwezo wa kuzoea na kuleta mabadiliko ni muhimu sana kwa kila mmoja kustawi haraka kwa huu ulimwengu unaobadilika kila kuchao. Ashoka anaandaa jamii ya kilimwengu yenye msingi ambapo kila mmoja ni mwanamageuzi. Katika nyoyo za kila mmoja,Vuguvugu la Wanamabadiliko wana maono ya kubadilisha jinsi Watoto na vijana wanakua na kupata ujuzi wa kuleta mabadliko kwa mujibu wa wote.

**www.ashoka.org**

## Kuhusu Worldreader

Worldreader inaamini kuwa wasomi hujenga ulimwengu bora. Tunafanya kazi na washikadau ulimwengu mzima na kuwasaidia watu pamoja na jamii zilizopo katika mazingira dhaifu kwa usomi wa kidijitali ambao husaidia kuimasirisha kusoma na kuandika na matokeo ya kujifunza kwa Watoto.

**www.worldreader.org**

2021 Ashoka na Worldreader

Kazi hii imetolewa kibali na Creative Commons Attribution-NonCommercial 4.0 International License

Kwa ujumbe zaidi tafadhali wasaliana na **privacy@ashoka.org** ama **publishing@worldreader.org**